



HAKIKA ZA HARAKA

Kuelewa Jinsi ya Chagua Mpango wa Bima ya Afya

Vidokezo katika karatasi hii ya hakika vitakusaidia kuchagua mpango wa bima ya afya kulingana na vipengele vilivyo muhimu kwako.



Mtandaoni katika nystateofhealth.ny.gov



Kwa simu kupitia
1-855-355-5777

TTY
1-800-662-1220

Hapa kuna vitu 6 vya kufikiria unapochagua mpango wa bima ya afya:

1 Ada

Hii ndio malipo ya kila mwezi unayolipia mpango wa bima ya afya, baada ya kupata usaidizi wowote wa kifedha unaostahiki kwa kupitia Soko. Unalipa ada hii kila mwezi, iwe unatumia huduma za kimatibabu au la. Kwa jumla jinsi ada ilivyo kubwa, ndivyo utakavyolipa kiwango kidogo cha kujigharamia unapopata huduma.

2 Gharama za kujigharamia

Hizi ni gharama unazolipia ukipata huduma ya kimatibabu. Vitu kama:

- **Yanayo punguzwa** - unalipa hii kwanza. Hiki ni kiwango unacholipa kabla ya mpango wako wa bima ya afya kuanza kulipia huduma. Mipango mingine ya bima hayana ya kupunguzwa.
- **Malipo ya ushirikiano** - unalipa kiwango kisichobadilika kwa kila ziara kwa daktari, dawa, au huduma nyingine, nao mpango wa bima ya afya unalipia yale mengine yote.
- **Bima ya ushirikiano** - unalipa asilimia fulani ya gharama, nao mpango wa bima ya afya unalipa unalipia yaliyosalia. Sio mipango yote ya bima ya afya ina bima ya ushirikiano.
- **Kiwango cha juu zaidi unachojigharimia** - kiwango cha juu zaidi unachohitaji kulipa kwa mwaka mmoja - muhimu sana! Mipango yote ya bima ya afya iliyoko Sokoni ina kiwango cha juu zaidi unachojigharimia mwenyewe.

3 Viwango 4 vya Chuma

Mipango imepangwa katika viwango 4 tofauti vya chuma. Viwango hivi yya chuma vinakupa dhana ya kile utahitajika kulipa.

Viwango vya chuma	Ada	Gharama za kujigharamia
Mipango ya Platinamu:	Juu Zaidi	Chini Zaidi
Mipango ya Dhahabu:	Juu Kidogo	Chini Kidogo
*Mipango ya Fedha:	Wastani	Wastani
Mipango ya Shaba:	Chini Zaidi	Juu Zaidi

*Kwa watu wengine, kulingana na mapato yao, kiwango cha Fedha huenda kikawa chaguo bora zaidi kwa sababu usaidizi wa kifedha unapatikana ili kupunguza gharama unazojigharamia.

ZAIDI >

4 Huduma Zinazosimamiwa

Fikiria kuhusu kana kwamba unataka huduma za ziada. “Mipango wastani ya bima” inasimamia huduma 10 sawia na pia gharama unazojiharimia ni sawia. Tofauti kati ya “mipango wastani ya bima” inayotolewa na kampuni tofauti ni mtandao wa watoa huduma, namna ya kupewa dawa na ada. “Mipango isiyo wastani ya bima” wakati mwingine inasimamia huduma za ziada kama vile huduma ya meno na macho kwa watu wazima.

5 Madaktari katika mtandao

Kila mpango wa bima ya afya una mkataba na madaktari na hospitali fulani. Inaweza kuwa ghali kutumia madaktari na hospitali zilizo nje ya mtandao. Kagua kuona kama madaktari wako wako katika mtandao.

6 Namna ya Kupewa Dawa

Kagua namna ya kupewa dawa ya mpango wako wa bima ya afya, ili kuona kama dawa unazotumia zimesimamiwa na utalipa kiwango kipi kila wakati unapopata kuandikiwa dawa.

Chagua mpango wa bima ya afya kufikia tarehe 15 ya kila mwezi kwa bima inayoanzia tarehe 1 ya mwezi unaofuatia. Kumbuka kuwa, watu wengi ni lazima wajisajili wakati wa kipindi cha usajili wazi wa kimwaka.



Mtandaoni katika
nystateofhealth.ny.gov



Kwa simu kupitia
1-855-355-5777

TTY
1-800-662-1220